

SAFARI YA MBINGUNI.

By Enteshi Lukuliko

Bukooba Kahama

19.02.2015

0767907766/0784907766

♩ = 70

1. Ee Mungu uko wa pi Bwana tu o ko e du ni a i me cha fu ka
Sa fa ri ya mbi ngu ni i na tu cha nga nya mbe le ku na gi za ne ne

5

a ja bu twa shi ndwa ha ta ku te mbe a
to to ro mwe le ke o tu me po te za

2. Kukicha, kila sehemu ni matukio, watu wanachinjwa kama wanyama, vita nazo kila mahali.
Ajali, za kutisha ona zatokea, wengi wamekufa hatukonao, sababu yao madereva.
3. Magonjwa, mengi sana yanatumaliza, UKIMWI unatisha kama simba, unaua hata watoto.
Ee Mungu, yatosha sasa uliondoe, tunalia Baba utusamehe, tufike salama mbinguni.
4. Vikongwe, na albino watapatapa, wanawindwa usiku na mchana, wamekosa nini Ee Mungu.
Watoto wachanga wanatupwa chooni, wasichana wajiiza njiani, safari yetu yashangaza
5. Fitina, wivu na uchu wa madaraka, viongozi warumbana bungeni, madhara ni kumwagadamu.
Dhuluma, mnyonge haki yake haipo, mwenye pesa sasa aabudiwa, Ee Yesu urudi upesi.
6. Tazama, ndoa za jinsia moja sasa, zinahararishwa bila aibu, mme na mme waoana.
Aibu, ni fedheha kubwa kwa Muumba, ndege na wanyama watushangaa, kama Sodoma na Gomola.
7. Shetani, azidi kutufuata nyuma, tumechoka twahitaji msaada, gari letu layumbayumba
Ee Yesu, dereva mwema twakuhitaji, njoo ushikirie usukani, tufike salama mbinguni.